

Salamu kutoka VANUATU!

Vanuatu ni nchi ya kisiwa cha kitropiki huko Bahari ya Pasifiki. Zaidi ya watu mia tatu elfu wanaishi huko!



FEDHA MARIDADI

Vanuatu ina fedha za rangi angavu ambazo zinaonyesha mandhari kutoka kwenye maisha ya kisiwani na miti na wanyama wanaoishi hapo.



SHUGHULI

Mataji ya Maua

Kwa ajili ya tamasha na sherehe, watu huko Vanuatu wanavaa mataji ya rangi za maua. Kata **karatasi ya rangi** katika maumbo ya maua. Tengeneza tundu dogo katikati ya kila ua. Kata **uzi** mrefu vya kutosha kufunga kuzunguka kichwa chako. Yafunge maua ya karatasi kwenye uzi. Kisha fungua miisho ya uzi pamoja. Taji lako li tayari kuvaliwa!



Kitabu cha Mormoni kilitafsiriwa kwa Kibislama mwaka 2004. Tangu wakati huo, karibia zaidi ya watu 8,000 wamejiunga na Kanisa huko Vanuatu!


KITABU CHA MORMONI

Waumini wa Kanisa huko Vanuatu wanahudhuria ibada itolewayo na Mzee Gary E. Stevenson mnamo Agosti 2017.



KISIWA CHA TROPIKI

Vanuatu inajulikana kwa pwani zake maridadi na maji safi ya buluu. Baadhi ya pwani hata zina changarawe nyeusi!



LUGHA

Kibislama, Kingereza na Kifaransa ndiyo lugha rasmi. Karibu kila mtu anaongea Kibislama!



MAELEZO YA UPISHI

Keki ya Nazi

Keki ya nazi ni chakula maarufu huko Vanuatu. Hapa kuna maelezo ya upishi unaweza kujaribu!

1. Koroga $\frac{1}{2}$ **kikombe sukari** na $\frac{3}{4}$ **kikombe siagi iliyoyeyushwa** katika bakuli.
2. Ongeza **mayai 2** na uchanganye.
3. Changanya katika $\frac{1}{2}$ **kikombe unga**, **1 kikombe nazi iliyokunwa** na **hamira kijiko 1**.
4. Mwaga kwenye kioka mikate kilichopakwa mafuta na oka kwa dakika 20 kwa nyuzi 300°F (150°C).

Hakikisha unapata msaada wa mtu mzima!

Tangkyu



Hii inamaanisha "asante" kwa Kibislama!

VIELELEZO NA ANNA OLDROYD